

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA WIKI YA AFYA KITAIFA 2025**

**30 Machi, 2025, Dodoma**

Wizara ya Afya imeandaa maadhimisho ya Wiki ya Afya 2025 yatakayofanyika kwa mara ya kwanza kuanzia tarehe **3 hadi 8 Aprili 2025** katika maeneo mbalimbali nchini. Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni **“Tulipotoka, Tulipo na Tunapoelekea: Tunajenga Taifa Imara Lenye Afya”**.

Maadhimisho haya yanalenga kuangazia maendeleo yaliyopatikana katika Sekta ya Afya, changamoto zilizopo pamoja na mikakati ya kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wote. Aidha, maadhimisho haya yatakuwa ni fursa ya kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya katika kuhakikisha afya bora kwa kila mwananchi.

Maadhimisho haya yanajumuisha shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:

1. **Tarehe 4 Aprili 2025:** Mdahalo wa Kisayansi wa Sekta ya Afya utakaofanyika katika maeneo mbalimbali nchini, ukiangazia uvumbuzi na mafanikio katika sekta ya afya.
2. **Tarehe 5 Aprili 2025:** Matembezi ya pamoja yatakayohusisha wadau wa afya na wananchi kwa lengo la kuhamasisha mazoezi ya viungo katika kuchochea afya bora.
3. **Zoezi la Upimaji wa Afya:** Wananchi wote wataweza kupima afya zao bila malipo.
4. **Maonyesho ya Sekta ya Afya:** Maonyesho haya yatafanyika katika maeneo yote yanayoshiriki maadhimisho, yakilenga kuonyesha huduma, teknolojia na mafanikio ya Sekta ya Afya.
5. **Kilele cha Maadhimisho:** Kilele cha maadhimisho haya kitafanyika tarehe **8 Aprili 2025** katika Mkoa wa Dodoma, Ukumbi wa Jakaya Kikwete, ambapo wadau mbalimbali wataungana kusherehekea mafanikio ya Sekta ya Afya.

Maadhimisho haya yanawaleta pamoja Wananchi, Wataalam wa afya, wadau na Serikali ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na maendeleo endelevu ya Ustawi wa Taifa la Tanzania.

  
Jenista Mhagama  
**WAZIRI WA AFYA**